

Je, wajua kwamba umekuja hapa duniani kwa sababu maalumu?

Je, wajua kwamba kuna kazi maalumu uliyotumwa na Mungu

kuja kuifanya?

Je, wajua kwamba kuna mpango maalumu ambao Mungu amekuwekea hapa duniani uje kuukamilisha?

Je, wafahamu kwamba mafanikio yako yanajulikana kwa Mungu kabla ya kuwepo kwako hapa duniani?

Je, wajua kwamba wewe ni bidhaa ya Mungu na umetengenezwa ili kuja kulitawala soko? Unapaswa kutambua kuwa, Mungu hajakuumba uje kutaabika hapa duniani; kwa maana hakuna kampuni inayotengeneza bidhaa zake kwa lengo la kushindwa sokoni. Kampuni zote hulenga kufanikiwa kwa bidhaa zao sokoni, na ndiyo maana huweka chapa na majina yao kwenye bidhaa.

Wewe ni bidhaa ya Mungu, na juu yako ameweka chapa yake. "Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi."(mwanzo1:26).